JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**



# MWONGOZO WA TAIFA WA DAWATI LA ULINZI NA USALAMA WA MTOTO NDANI NA NJE YA SHULE

Dodoma

Juni, 2022

# Mwongozo Wa Taifa Wa Dawati La Ulinzi Na Usalama Wa Mtoto Ndani Na Nje Ya Shule

Juni, 2022

# YALIYOMO


**TAFSIRI YA MANENO** iv

**SHUKRANI** v

**DIBAJI** vii

**USULI** ix

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** 1

1.1. Utangulizi 2

1.2. Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule 3

1.3. Umuhimu wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto 4

1.4. Malengo ya Mwongozo 5

1.4.1. Lengo Kuu 5

1.4.2. Malengo Mahsusi 5

1.5. Wigo wa matumizi ya Mwongozo 6

**SURA YA PILI: UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA DAWATI LA ULINZI NA USALAMA WA MTOTO NDANI NA NJE YA SHULE** 7

2.1. Dhana ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule 8

2.2. Muundo wa Dawati 8

2.3. Uendeshaji wa Dawati 9

2.3.1. Kanuni za uendeshaji wa Dawati 9

2.3.2. Kujali 11

2.3.3. Utaratibu wa utoaji wa taarifa za ukatili kupitia Dawati la Ulinzi wa Mtoto Shuleni 11

2.3.3.1. Mtu mmoja mmoja 11

2.3.3.2. Baraza la wanafunzi 11

2.3.3.3. Sanduku la Maoni Dhidi ya Vitendo vya Ukatili 12

2.3.4. Hatua za kushughulikia taarifa za vitendo vya ukatili shuleni 13

2.3.5. Rufaa 15

2.3.6. Elimu kuhusu ukatili 15

2.3.7. Huduma za Malezi na Unasihi. 16

2.3.8. Mazingira yanayofaa kwa unasihi 17

**SURA YA TATU: MGAWANYO WA MAJUKUMU 18**

3.1. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum 19

3.2. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia 19

3.3. Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) 20

3.4. Wadau wa Maendeleo 21

3.5. Tawala za Mikoa 22

3.6. Mamlaka za Serikali za Mitaa 23

3.6.1. Halmashauri 23

3.6.2. Kata 23

3.6.3. Serikali ya Kijiji/Mtaa 24

3.6.4. Kamati na Bodi ya Shule 24

3.6.5. Mkuu wa Shule 25

3.6.6. Walimu wa Malezi na Unasihi 25

3.6.7. Jamii 26

3.6.8. Viongozi wa Dini /Taasisi za Dini 27

3.6.9. Marafiki wa Elimu 27

**SURA YA NNE: URATIBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI 28**

4.1. Uratibu 29

4.2. Ufuatiliaji 29

4.3. Tathmini 30

**HITIMISHO 31**

# TAFSIRI YA MANENO

| | |
|---|---|
| **Mtoto** | Kwa mujibu wa Sheria ya mtoto Na. 21 (2009) mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. |
| **Mkuu wa Shule** | Mkuu wa Shule ni kiongozi Mkuu wa Shule ya Msingi au Sekondari. |
| **Dawati la ulinzi wa Watoto shuleni** | Jukwaa la watoto katika shule za msingi na sekondari linaloshughulikia masuala ya ukatili. |
| **Ukatili:** | Kitendo chochote anachofanyiwa mtoto au watoto kinachoweza kuleta madhara ya kimwili, kiakili, kingono na kisaikolojia. |
| **Wadau** | Wizara, Taasisi za umma, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, Sekta binafsi, Jamii, watu binafsi ambao watatekeleza Mwongozo huu, |
| **MTAKUWWA** | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto |
| **Watoto wenye mahitaji maalum** | Watoto wanaoishi na aina mbalimbali za ulemavu |
| **Watumishi wa shule** | Wafanyakazi wote ambao siyo walimu ndani ya shule |
| **Ulinzi wa mtoto** | Mfumo wa kuhakikisha usalama wa mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili. |
| **Unasihi** | Msaada wa ushauri wa kitaalamu unaotolewa kwa mtoto ambaye anakabiliwa na msongo wa mawazo au vitendo vya ukatili. |
| **Rufaa** | Utaratibu wa kupeleka shauri kutoka kwa mtoa huduma mmoja kwenda kwa mtoa huduma mwingine au kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine kwa ajili ya huduma au suluhu zaidi. |
| **Wigo** | Maeneo ambayo mwongozo unatumika. |
| **Rafiki wa Elimu** | Mtu yeyote anayejitolea kutetea haki ya elimu ya mtoto na kumlinda mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili akiwa nyumbani, njiani kwenda na kurudi shuleni |

# SHUKRANI

Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni na nje ya shule ni mojawapo ya afua za utekelezaji wa Mpango kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Aidha, mwongozo huu umeandaliwa kwa lengo la kuwashirikisha Watoto katika masuala yanayohusu Ulinzi na Usalama wao hususani katika eneo la kutoa taarifa ya dalili za kufanyiwa ukatili au taarifa za ukatili wanaofanyiwa watoto wanapokuwa nyumbani, maeneo ya wazi wakiwa wanaenda au kurudi shuleni na katika mazingira ya shule.

Mwongozo huu umeandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wakiwemo watoto wenyewe, Wizara za Kisekta na Taasisi za Serikali, Mashirika ya Kimataifa na Asasi zisizo za Kiserikali kwa lengo la kumshirikisha Mtoto katika ulinzi na usalama wake kama ilivyoainishwa katika Sera, Sheria na Mikataba ya Kimataifa na Kikanda inayohusu ulinzi wa Mtoto.

Wizara inatoa shukrani za pekee kwa Mashirika yaliyoshiriki katika kufanilisha uandaaji wa Mwongozo huu ikiwa pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la HakiElimu, Plan International, Save the Children International, Grace Community Development and Education, Peoples Development Forum, RAFIKI-Social Development Organization, SOS Village Tanzania, Youth Education Through Sports Tanzania kwa michango yao ya hali na mali iliyowezesha kukamilika kwa Mwongozo huu.

Aidha, Wizara inatoa rai kwa wadau wote wanaohusika katika kuanzisha na kuratibu Dawati la Ulinzi wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari kutumia Mwongozo huu ili kuwa na sura na muundo unaofanana wa uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Watoto Ndani na Nje ya Shule. Kwa namna ya pekee,

Serikali inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliooneshа utayari wa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha watoto wetu wanajengewa uwezo wa kujilinda na wanalindwa dhidi ya ukatili wa aina yoyote.



Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb)

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# DIBAJI

Mwongozo wa Taifa wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni na kwenye Jamii umeandaliwa kwa ajili ya kutoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali na Wadau wengine wa ulinzi wa Watoto katika kuanzisha na kuimarisha usalama wa Watoto nchini. Serikali, kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeandaa Mwongozo wa Taifa wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule na nje ya shule ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mwongozo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya shule na vyuo vya ualimu ulioanza kutumika Mwaka 2020. Mwongozo huo una lengo la kuimarisha malezi, ulinzi na unasihi kwa ajili ya watoto katika shule za msingi na sekondari na kuhakikisha kwamba Mtoto anapata elimu na ujuzi katika mazingira salama na rafiki bila aina yoyote ya ukatili.

Katika kumshirikisha Mtoto kwenye ulinzi na usalama wake, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule ili kuwezesha watoto kushiriki katika kutoa taarifa za dalili zozote za ukatili na kumsaidia Mtoto aliyefanyiwa ukatili ili kupata huduma stahiki. Aidha, Mwongozo huu ni utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Ulinzi wa Mtoto na Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18-2021/22).

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kushirikisha Wadau mbalimbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wataalam kutoka Wizara za Kisekta, Mashirika ya Umoja wa Mataifa hususan UNICEF na WHO, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wataalam kutoka Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao ndio watekelezaji wakuu wa afua za ulinzi wa watoto shuleni, na kwenye jamii.

Katika kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa Mwongozo huu, Wizara inahimiza Wadau wote wa masuala ya ulinzi na usalama wa Watoto katika ngazi mbalimbali kuutumia Mwongozo huu katika uundaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Watoto Ndani na Nje ya Shule ili kuwa na sura na muundo unaofanana wa Madawati hayo katika Halmashauri na Mikoa yote nchini.



Dkt. Zainabu A. S. Chaula

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# USULI

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa masuala ya watoto imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ndani na nje ya shule. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, iliandaa na kusambaza Waraka wa Elimu Na.11 wa Mwaka 2002 uliotoa mwongozo wa kuanzisha huduma ya malezi na unasihi katika shule na vyuo vya ualimu na Waraka wa Elimu Na. 24 wa Mwaka 2002 kuhusu utaratibu wa utoaji wa adhabu ya viboko shuleni kwa ajili ya kupunguza athari za ukatili dhidi ya watoto na kudhibiti adhabu za viboko kwa wanafunzi. Katika kuimarisha ulinzi na malezi ya watoto shuleni, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya shule na vyuo vya ualimu ulioanza kutumika Mwaka 2020 kwa lengo la kuimarisha malezi, ulinzi na unasihi kwa ajili ya watoto katika shule za Msingi na Sekondari na kuhakikisha kwamba mtoto anapata elimu na ujuzi katika mazingira salama na rafiki bila aina yoyote ya ukatili.

Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto ndani ya shule na kwenye Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikihusisha na Wadau wengine wa masuala ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto imeandaa Mwongozo wa Taifa wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni na kwenye Jamii lengo likiwa ni kumshirikisha Mtoto katika kutoa taarifa za dalili za kufanyiwa ukatili na taarifa za ukatili wa aina zote dhidi yake ndani na nje ya shule.

Uratibu na usimamizi wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto utafanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Elimu Kata kwa usaidizi wa walimu wa Malezi na Unasihi kwa uangalizi wa Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu. Ni wajibu wetu sote, Serikali, Taasisi zisizo za Kiserili na Wadau wote kuhakikisha

kwamba Mwongozo huu unatumika katika uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto shuleni na nje ya shule katika shule zote za Msingi na Sekondari kwa kuwashirikisha watoto wenyewe ili na watoto washiriki katika kukabilliana na vitendo vya ukatili dhidi yao. Usalama wa mtoto ndani na nje ya shuleni utamfanya Mtoto kusoma bila vikwazo vinavyoweza kumzorotesha katika masomo yake au kuacha shule.



Prof. Eliamani Sedoyeka

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# Sura ya Kwanza:

# Utangulizi

## 1.1. Utangulizi

Ukatili dhidi ya watoto katika mazingira ya ndani na nje ya shule ni mojawapo ya sababu inayochangia baadhi ya watoto kuacha shule, na kujihusisha na shughuli hatarishi ambazo nyingi hazina manufaa kwa maendeleo yao binafsi, familia, jamii na Taifa. Vilevile, watoto wanaofanyiwa ukatili wana uwezekano mkubwa wa kuendeleza vitendo vya ukatili wanapokuwa watu wazima na hii inasababisha mnyororo wa ukatili kuendelea. Vitendo vya ukatili vinasababisha kuongezeka kwa gharama kubwa za afya, elimu, huduma za mahakama na kupunguza pato la kaya na Taifa. Watoto wanahitaji ulinzi na malezi bora ili kuwajenga kimwili na kiakili kwa manufaa na maendeleo yao.

Takwimu za Jeshi la Polisi za Mwaka 2021 zinaonesha kuwa jumla ya matukio ya ukatili kwa watoto yaliyotolewa taarifa katika vituo vya polisi ni 11,499 ambapo Mikoa inayoongoza kwa ukatili ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Ilala (489). Makosa yanayoongoza kwa idadi ni matukio ya ubakaji (5,899) Mimba kwa wanafunzi (1,677), Ulawiti (1,114), Kukatisha masomo (790) na Shambulio la kimwili (390). Aidha, Takwimu za Elimu (BEST 2020) zinaonyesha kuwa, jumla ya wanafunzi 1,135 wa shule za msingi na wanafunzi 5,340 wa katika shule za sekondari waliacha masomo kwa sababu ya ujauzito. Mikoa yenye takwimu za juu kwa mimba za utotoni kwenye shule za msingi ni Mwanza (98), Tanga (97), Ruvuma (84), Geita (78) na Morogoro (71), wakati kwenye shule za sekondari ni Mwanza (491), Morogoro (389), Dodoma (381), Mara (369) na Ruvuma (327). Ikumbukwe kwamba, katika utafiti wa hali ya ukatili nchini uliofanywa na shirika la UNICEF Mwaka 2011 ulionyesha kwamba kiwango cha ukatili shuleni na nyumbani ni uwiano wa asilimia 40 kwa 60.

Katika kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, serikali imechukua hatua kadhaa ili kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto shuleni na nje ya shule ikiwa ni pamoja na ;

i. Kusaini na kuridhia mikataba ikiwemo Mkataba wa Haki za Binadamu wa Mwaka 1948, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto wa Mwaka 1989, Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990,

ii. Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 pamoja na kutunga Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 na marekebisho yake ya Mwaka 2019. Jitihada nyingine ni

iii. Kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto katika Mikoa 26 na Halmashauri 184, Vituo vya Mkono kwa Mkono 13 katika mikoa 10 ya Tanzania Bara (2021),

iv. Kuanzisha nyumba Salama 9 katika mikoa 7(2021) na Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo vya Polisi 421 nchini (2021) .

v. Katika kushughulikia ukatili dhidi ya watoto shuleni, Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliandaa Waraka wa Utaratibu wa Utoaji wa Adhabu wa Mwaka 2002 na Mwaka 2020 ilipitisha Mwongozo (Waraka) wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Watoto katika Shule na Vyuo vya Elimu kwa lengo la kuweka mazingira rafiki na salama ya kujifunza na kufundishia kwa wanafunzi na walimu.

Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeweka kipaumbele katika kutokomeza ukatili dhidi ya watoto shuleni na kwenye jamii, na hivyo imeandaa Mwongozo huu kuongeza nguvu kwenye utekelezaji wa Afua za kutokomeza ukatili katika maeneo hayo.

## 1.2. Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule

Dawati la Ulinzi na Usalama katika kila shule ya msingi na sekondari ni jukwaa la watoto kujadili, kupeana taarifa za kujilinda dhidi ya

vitendo vya ukatili, na namna ya kutoa taarifa za ukatili ili ziweze kushughulikiwa na walimu wa malezi kupitia rufaa. Kwa kuwa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto linaratibiwa kuanzia kila Kijiji/Mtaa kupitia mfumo uliowekwa na MTAKUWWA, unatilia mkazo kuboreshwa kwa vituo vya rufaa na uwajibikaji wa vyombo husika ili kuhakikisha jitihada endelevu za utekelezaji wa Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto shuleni, kwenye vyuo vya elimu, pamoja na kwa watoto walio ndani na nje ya shule, unafanyika katika ngazi zote.

## 1.3. Umuhimu wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya Mwaka 2009 kila Mtoto anayo haki ya kuishi na kupata malezi bora, ulinzi na kuendelezwa bila aina yoyote ya ubaguzi. Mtoto anapokuwa nyumbani au kwenye jamii anapaswa kulindwa dhidi ya matukio ya ukatili na kuhakikishiwa usalama wake. Aidha, mtoto anapokuwa shuleni anapaswa kuandaliwa mazingira rafiki na tulivu ya kujifunza taaluma mbalimbali ili kuweza kuwa mbunifu na kupata ujuzi utakaomsaidia kujikimu kiuchumi na kuchangia pato la Taifa katika siku za usoni.

Athari ya ukatili dhidi ya watoto inapelekea kuongezeka kwa idadi kubwa ya watoto wanaoacha shule, kujiingiza kwenye mambo yasiyokuwa na tija au manufaa kwao na jamii kwa ujumla, hivyo kupunguza ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kusababisha upungufu wa nguvu kazi ya Taifa. Ukatili dhidi ya watoto una madhara makubwa kwa mtoto kiafya, kiakili na kiuchumi, lakini pia una athari kwa wazazi/walezi, jamii na serikali kwani pale mtoto atakapokuwa ameathirika kiafya au atakapopata mimba anakuwa mzigo kwa wazazi/walezi wake na jamii kwa ujumla. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanyika kutokomeza ukatili dhidi ya watoto, vitendo hivyo vimeendelea kutolewa taarifa katika maeneo mbalimbali nchini. .Katika kukabiliana na changamoto za ukatili dhidi ya watoto ndani

na nje ya shule, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaweka mkakati jumuishi wa kushirikisha Wizara za Kisekta na Wadau katika masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto, kuimarisha mfumo wa kuzuia matukio ya ukatili yasitokee shuleni kama ilivyoainishwa kwenye MTAKUWWA. Kuandaliwa kwa Mwongozo huu kunaimarisha juhudi za Serikali katika ngazi zote kuanzia ngazi ya Taifa hadi ya Kijiji/Mtaa, kushirikiana na wananchi, wadau wa maendeleo, viongozi wa dini, vyombo vya ulinzi na wengine wote kama ilivyoainishwa kwenye MTAKUWWA, kuweka na kuimarisha mifumo ya ulinzi wa Mtoto shuleni na nje ya shule.

## 1.4. Malengo ya Mwongozo

### 1.4.1. Lengo Kuu

Kuweka mfumo wa ulinzi na usalama wa Mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili shuleni na katika jamii.

### 1.4.2. Malengo Mahsusi

i. Kuweka utaratibu wa uanzishaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari.

ii. Kuweka utaratibu rafiki kwa watoto kutoa taarifa za vitendo vya ukatili shuleni.

iii. Kuweka utaratibu wa kushughulikia mashauri ya ukatili unaofanyika ndani na nje ya shule.

iv. Kuimarisha huduma za ushauri nasaha na unasihi kwa watoto zitakazotolewa shuleni.

v. Kuwajengea uwezo wajumbe wa Dawati na walimu wa malezi na unasihi katika kutoa huduma za malezi, unasihi na ulinzi wa watoto shuleni.

vi. Kuainisha majukumu ya kila mdau atakayehusika katika utekelezaji wa Mwongozo huu.

vii. Kufanya ufuatiliaji, tathmini ya uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Watoto shuleni.

viii. Kuongeza matokeo chanya katika maendeleo ya watoto kitaaluma shuleni

## 1.5. Wigo wa matumizi ya Mwongozo

Mwongozo huu utatumika katika shule za msingi na sekondari pamoja na mazingira ya nje ya shule katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Mwongozo utatumiwa na wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu kufahamu jinsi ya kuzuia na kukabiliana na vitendo vya ukatili katika mazingira ya shule. Vilevile, Mwongozo huu utatumiwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi na Walimu wa malezi na Maafisa Elimu katika kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Dawati.

Aidha, Mwongozo huu utatumika kuwajengea uwezo wazazi, uongozi wa shule, Bodi na Kamati ya shule kuhusu vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto ndani na nje ya shule ili wao kama sehemu ya wazazi na walezi wasaidie katika kushughulikia changamoto wanazokumbana nazo watoto katika kuimarisha shughuli za Dawati. Vilevile, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi na Maafisa Elimu katika ngazi za Taifa, Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji/ Mtaa watatumia Mwongozo huu kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Dawati.

# Sura ya Pili:

# Uanzishaji na Uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule

## 2.1. Dhana ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule

Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto ni jukwaa linaloanzishwa katika shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuzuia na kushughulikia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Dawati hili ni mojawapo ya afua za ulinzi wa watoto ndani na nje ya shule na litasaidia kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili.

## 2.2. Muundo wa Dawati

Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto litaundwa katika shule za Msingi na Sekondari ambapo litajumuisha walimu wa malezi na unasihi pamoja na wanafunzi Vinara watakaochaguliwa miongoni mwa wanafunzi wote kwa mchanganuo ufuatao:

i. Katika shule za msingi kutakuwa na walimu wa malezi na unasihi wawili (Me na Ke) ambao watakuwa waratibu na wasimamizi wa Dawati. Wajumbe 15 kutoka miongoni mwa wanafunzi kuanzia darasa la kwanza, pili, tatu, tano na la sita ambapo watachaguliwa wajumbe wawili kwa kila darasa kwa uwiano wa jinsi, ikijumuisha watoto wawili wenye mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu (kike na kiume) ambao watajumuika na walimu wa malezi na unasihi ili kuunda Dawati. Dawati pia litakuwa na mwakilishi mmoja kutoka kamati ya shule.

ii. Katika shule za sekondari kutakuwa na walimu wa malezi na unasihi wawili (Me na Ke,) ambao watakuwa waratibu na wasimamizi wa Dawati. Wajumbe wasiopungua 11 kutoka miongoni mwa wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu pamoja na kidato cha tano, ikiwa ni wajumbe wawili kwa kila darasa, kwa uwiano wa jinsi ikijumuisha watoto wawili wenye mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu (kike na kiume) ambao watajumuika na walimu wa

malezi na unasihi. Dawati katika shule ya sekondari litakuwa na mwakilishi mmoja kutoka Bodi ya shule.

iii. Wanafunzi (Wajumbe) watachaguliwa kila mwaka ili kujenga uelewa kuhusu masuala ya ukatili kwa wanafunzi wengi shuleni.

iv. Wanafunzi (Wajumbe) wawili wenye mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu (kike na kiume) ambao watajumuika kuunda Dawati watatoka darasa lolote iwapo watakuwepo kwenye shule husika.

## 2.3. Uendeshaji wa Dawati

### 2.3.1. Kanuni za uendeshaji wa Dawati

Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto ndani na nje ya Shule litaendeshwa kwa kufuata kanuni za ulinzi wa mtoto ambazo ni:

**i.** **Maslahi ya mtoto;** Sheria inaelekeza kwamba, hatua zozote zitakaazochukuliwa katika kushughulikia mashauri ya mtoto lazima kipaumbele cha kwanza kiwe ni haki na ulinzi wa mtoto.

**ii.** **Ushirikishwaji wa mtoto;** maoni ya mtoto yapewe nafasi na yaheshimiwe wakati wa kutoa huduma kwa kuzingatia jinsi, umri na uelewa wa mtoto.

**iii.** **Haki za mtoto;** afua zote za haki za mtoto zitahusisha watendaji wa Serikali katika ngazi mbalimbali pamoja na wadau wengine, watoa huduma, wazazi/walezi na watu wengine wanaowajibika kutimiza majukumu na wajibu wao katika kusimamia haki za watoto.

**iv.** **Haki za binadamu;** haki za mtoto ni sehemu ya haki za binadamu, hivyo wadau wa watoto wana wajibu wa

kutekeleza na kusimamia utoaji wa haki za msingi kama ilivyoelekezwa na Sera ya Mtoto (2008), Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (UN-CRC) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) kwa ajili ya ustawi wa mtoto.

v. **Ushiriki wa familia katika ulinzi wa mtoto;** afua za ulinzi wa mtoto shuleni zinatakiwa zifanyike sambamba na ushirikishwaji wa familia za watoto ili kupunguza misuguano, unyanyapaa na kukosekana kwa amani kwenye familia. Aidha, afua hizo zihusishe watoto waliofanyiwa ukatili au walio katika hatari ya kufanyiwa ukatili.

vi. **Usiri;** taarifa zote zinazomlenga mtoto zinatakiwa zitunzwe kwa siri. Uongozi wa Dawati na shule unawajibika kutunza siri husika wakati wote wanapowasiliana na taasisi nyingine kuhusu utatuzi wa changamoto za mtoto.

vii. **Uaminifu;** Wajumbe wa Dawati wanatakiwa kuwa waaminifu kwa mashauri wanayoyapokea, kuyachambua na kuyafanyia kazi.

viii. **Haki na usawa;** watoa huduma wanapaswa kuzingatia misingi ya haki, utu, umri na usawa wa kijinsia wakati wote wa utoaji huduma kulingana na muktadha wa Mwongozo huu.

ix. **Rufaa na Huduma;** Walezi wa Dawati wanapaswa kutoa huduma kulingana na mipaka ya utaalamu wao katika kushughulikia taarifa za ukatili zilizowasilishwa na kutoa rufaa kwa matukio ambayo yako nje ya uwezo wao kwa kuzingatia umri na usawa wa kijinsia.

### 2.3.2. Kujali

Walimu, wazazi/walezi na watendaji wengine wanatakiwa kujali na kuchukua hatua ya kuwalinda watoto bila kuonesha hali ya mshangao na mshituko baada ya kupokea taarifa za vitendo vya ukatili ili waweze kuchukua hatua ya kuwalinda watoto hao**.**

### 2.3.3. Utaratibu wa utoaji wa taarifa za ukatili kupitia Dawati la Ulinzi wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule

Taarifa za ukatili dhidi ya mtoto ndani na nje ya shule zinaweza kutolewa kupitia;

#### 2.3.3.1. Mtu mmoja mmoja

Walimu wa malezi na unasihi waelekeze wanafunzi namna ya kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili vinavyohusu wao wenyewe au wanafunzi wenzao katika mazingira ya shule na katika jamii. Taarifa hizo zinaweza kufikishwa kwa wajumbe wa Dawati, mwalimu wa malezi na unasihi au Mwalimu Mkuu/Mkuu wa Shule punde kitendo hicho kinapotokea au kipo katika hatari ya kutokea. Pia katika ngazi ya jamii taarifa zinaweza kufikishwa kwa viongozi wa Kijiji/Mtaa au Maafisa Ustawi wa Jamii/ Maendeleo ya Jamii waliopo katika eneo husika. Walimu na watumishi wasio walimu watatoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa walimu wa malezi na unasihi au Mwalimu Mkuu na iwapo kitendo cha ukatili kitafanywa na mmoja kati ya walimu au mtumishi asiye mwalimu. Aidha, taarifa hiyo itafikishwa kwa Mkuu wa Shule na kupelekwa kwenye Kamati/Bodi ya shule.

#### 2.3.3.2. Baraza la wanafunzi

a. Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto litaitisha Baraza la Wanafunzi utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) chini ya usimamizi wa mwalimu wa malezi na unasihi kujadili vitendo vya ukatili vinavyotokea ndani na nje ya shule ili kujadili hali

ya ukatili kwa kipindi husika. Mwalimu wa malezi na unasihi atashirikiana na viongozi wa Dawati kupanga ratiba ya vikao pamoja na ajenda zake ili vifahamike kwa wanafunzi pamoja na walimu wote shuleni;

b. Tangazo la Baraza la wanafunzi litabandikwa sehemu mbalimbali ili Wanafunzi wafahamu na mkutano huo utaongozwa na Mwenyekiti wa Dawati na mwalimu wa malezi na unasihi atakuwepo kwa ajili ya ushauri.

c. Wajumbe wa Dawati watahakikisha kwamba, kunakuwepo na karatasi na peni kwa ajili ya watoto kuandika maoni yao. Wajumbe wa Dawati watahamasisha wanafunzi kupeleka malalamiko na taarifa za vitendo vya ukatili vinavyotokea shuleni.

**2.3.3.3. Sanduku la Maoni Dhidi ya Vitendo vya Ukatili:**

Sanduku la Maoni katika shule za msingi na sekondari litatumika na wanafunzi kuwasilisha taarifa za matukio ya ukatili yanayowakabili wakiwa ndani na nje ya shule. Utaratibu wa matumizi ya Sanduku la Maoni dhidi ya vitendo vya ukatili shuleni utakuwa kama ifuatavyo:

a. Kutolea taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto litaanzishwa katika kila shule nchini.

b. Mkuu wa Shule kwa kushirikiana na mwalimu wa malezi na unasihi awaeleze wanafunzi wote uwepo na umuhimu wa sanduku la kutolea taarifa za vitendo vya ukatili shuleni. Mwalimu awape uhuru watoto wachague sehemu inayofaa kuweka sanduku la taarifa za ukatili.

c. Mkuu wa Shule pamoja na wanafunzi wakubaliane na waandae sehemu ambayo itakuwa rahisi na salama kufikika kwa usiri na bila woga kwa watoto wote, wakiwemo wenye ulemavu, pamoja na watumishi wasio walimu na wanajamii,

kwa ajili ya kuweka taarifa za ukatili.

d. Utaratibu wa usimamizi wa sanduku la vitendo ya ukatili utatolewa kwa wajumbe wa Dawati na walimu wa malezi na unasihi waliopo shuleni.

e. Wanafunzi waelezwe kuwa, iwapo taarifa anayotoa inahitaji msaada wa haraka ni vema wafikishe taarifa hiyo moja kwa moja kwa mwalimu wa malezi na unasihi.

**Angalizo**

Wakati wa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili ndani na nje ya shule, yafuatayo yazingatiwe:

i. Wapokea taarifa waepuke maswali yenye viashiria vya vitisho wakati wa kuhoji;

ii. Watoa taarifa wajengewe mazingira rafiki ili wawe huru kutoa taarifa zilizo sahihi;

iii. Utoaji wa taarifa zote za ukatili unatakiwa kuwa wa siri ili kulinda haki na maslahi ya mtoto na pia itasaidia kupunguza unyanyapaa kwa watoto na

iv. Kama Mtoto atafanyiwa ukatili ambao unaweza kupelekea hatari ya kupoteza maisha, taarifa hizi zifikishwe moja kwa moja kituo cha polisi.

### 2.3.4. Hatua za kushughulikia taarifa za vitendo vya ukatili shuleni

Katika kushughulikia mashauri ya vitendo vya ukatili shuleni hatua zifuatazo zitazingatiwa:

i. Sanduku la Maoni litakuwa na kufuli tatu (3). Funguo zitatunzwa na mwalimu wa malezi na unasihi na wajumbe 2

wa Dawati la Ulinzi.

ii. Sanduku litafunguliwa mara tatu (3) kwa wiki na kila linapofunguliwa wajumbe wanne (4) watatakiwa kuwepo wakiwemo, wawakilishi wawili wa wanafunzi na Walimu wawili (Ke na Me) wa malezi na unasihi.

iii. Sanduku likishafunguliwa, kero na maoni yote yatasomwa na kuorodheshwa katika daftari maalum ambalo litatunzwa kwa siri na mwalimu wa malezi na unasihi.

iv. Walimu wa malezi na unasihi wataandaa taarifa ya hali ya ukatili shuleni na kuifikisha kwa Mwalimu Mkuu naye ataifikisha taarifa hiyo kwenye kamati ya shule, serikali ya Kijiji/Mtaa na hatimaye kwenye halmashauri ya wilaya kwa hatua zinazostahili Aidha, wakati mwingine taarifa itawasilishwa kwenye ngazi husika kulingana na tatizo au changamoto iliyojitokeza. Ngazi hizo ni kama vile Dawati la Jinsia, Wanawake na Watoto la Jeshi la Polisi, kamati za MTAKUWWA na Ofisi za Ustawi wa Jamii.

v. Dawati litakuwa na jukumu la kutoa mrejesho kwa wanafunzi kuhusu hatua zilizochukuliwa kwa masuala yasiyo ya faragha.

vi. Walimu wa malezi na unasihi kwa kushirikiana na wazazi wa Mtoto aliyeathirika watatoa huduma za ushauri na unasihi, msaada wa kisaikolojia wa awali pamoja na rufaa kulingana na uhitaji wa Mtoto aliyefanyiwa ukatili akiwa ndani au nje ya shule. Matukio yaliyo juu ya uwezo wao yatawasilishwa katika kamati ya shule na hatimaye serikali ya kijiji/mtaa kwa hatua zaidi.

vii. Walimu wa malezi na unasihi watafanya ufuatiliaji wa rufaa walizozitoa na kuendelea na ushauri na unasihi pamoja na msaada wa kisaikolojia kwa watoto waliofanyiwa vitendo

vya ukatili.

### 2.3.5. Rufaa

Rufaa za mashauri ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto shuleni zitafanyika ili kumsaidia Mtoto mhanga wa vitendo vya ukatili kupata huduma za msaada wa kisaikolojia, ushauri, unasihi sheria na tiba.Maeneo muhimu kwa rufaa za mashauri ya vitendo vya ukatili kwa watoto shuleni yatakuwa kama ifuatavyo;

i. Mkuu wa shule husika

ii. Ofisi za Ustawi wa Jamii(Halmashauri)

iii. Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya Mtaa/ Kata

iv. Dawati la Jinsia, Wanawake na Watoto la Jeshi la Polisi liliopo kituo cha polisi cha karibu

v. Kituo cha afya na zahanati kilichopo karibu

vi. Ofisi za msaada wa kisheria iliyopo karibu

vii. Nyumba Salama iliyopo karibu

viii. Vituo vya Mkono kwa Mkono kilichopo karibu

ix. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

x. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

### 2.3.6. Elimu kuhusu ukatili

Dawati la ulinzi wa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili shuleni lina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanafahamu maana ya ukatili, aina za ukatili, sababu za ukatili na athari zake.

Wanafunzi wanapaswa kufundishwa mbinu sahihi zinazofaa kujilinda dhidi ya vitendo vya ukatili ndani na nje ya shule. Aidha, wanafunzi wataelekezwa umuhimu wa utoaji wa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili na hatua za kuchukua punde ukatili unapotokea au panapokuwa na viashiria vya ukatili kutokea ndani na nje ya shule.

Katika kuwezesha Dawati lifanye kazi kwa weledi, wanafunzi wanapaswa kuelewa dhana ya Dawati na uhusiano wao na walimu wa malezi na unasihi na watumishi wasio walimu katika kutokomeza ukatili shuleni.

Mafunzo kwa wajumbe wa Dawati yatatolewa kwa kufuata mada zitakazoandaliwa na Wizara yenye dhamana ya masuala ya watoto nchini. Miongozo itakayotumika kuandaa mada hizo ni pamoja na

i. Sheria ya Mtoto Na.21 ya Mwaka 2009, Kanuni za Usalama wa Mtoto ya Mwaka 2014;

ii. Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto Shuleni na Vyuo vya Ualimu Tanzania, Novemba, 2020;

iii. Kitini cha Elimu ya Malezi ya Familia Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania, Septemba, 2017;

iv. Kitini cha Mafunzo kwa Wawezeshaji wa Mabaraza ya Watoto Tanzania Mei, 2019

### 2.3.7. Huduma za Malezi na Unasihi

Mtoto aliyefanyiwa ukatili anastahili kupata huduma za malezi ikiwemo chakula, malazi, mavazi, uchangamshi, afya, elimu, ulinzi na usalama. Aidha, mtoto anahitaji kupatiwa huduma ya unasihi ili kumsaidia kujitambua kwa uwazi na kuelewa tatizo linalomkabili na kuchukua hatua stahiki za kutatua tatizo hilo.

### 2.3.8. Mazingira yanayofaa kwa unasihi

i. Kuwepo kwa chumba maalum kwa ajili ya walimu wa malezi na unasihi kuwezesha unasihi kufanyika kwa usiri na ufanisi zaidi;

ii. Kuwepo kwa muda maalum unaotambulika na wanafunzi ambapo huduma ya unasihi itatolewa. Ikitokea dharura, walimu wa malezi na unasihi wawe tayari kutoa huduma;

iii. Wanafunzi ndani na nje ya shule waelezwe uwepo na umuhimu wa huduma ya ushauri na unasihi kwa ajili ya ustawi wao hata kama hajafanyiwa ukatili. Kuwepo masanduku imara kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za siri za watoto waliopata huduma za malezi na unasihi; na

iv. Kuwepo kwa walimu 2 (Ke na Me) waliopata mafunzo ya ushauri na unasihi kulingana na miongozo ya Serikali. Mafunzo ya mara kwa mara kwa walimu wa malezi na unasihi ni muhimu ili waweze kwenda na wakati.

# Sura ya Tatu: Mgawanyo wa Majukumu

## 3.1. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Majukumu yafuatayo yatafanywa na Idra ya Maendeleo ya Mtoto na yatasimamiwa na Katibu Mkuu.

i. Kutoa maelekezo ya kisera, kisheria na miongozo kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule;

ii. Kuandaa na kuhuisha miongozo ya kufundishia kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule;

iii. Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa watalaam wa kisekta katika ngazi ya Kitaifa, Mikoa na Serikali za mitaa kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto shuleni;

iv. Kuratibu utekelezaji wa mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule;

v. Kufanya tathmini, kutoa taarifa na mrejesho kwa wadau kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule;

vi. Kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuwezesha uratibu na utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule; na

vii. Kuandaa moduli na vitini vya kufundishia watoto kuhusu ulinzi na usalama wao na kuvisambaza kwa watekelezaji katika sekretariati za mikoa, mamlaka ya serikali za mitaa na wadau.

## 3.2. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Majukumu yafuatayo yatafanywa na Afisa anayeshughulikia masuala ya watoto na yatasimamiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia chini ya Ofisi ya Kamishina wa Elimu

i. Kushirikiana na wizara za kisekta kuandaa moduli na vitini vya kufundishia kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto ndani na nje ya shule kwa kuzingatia miongozo;

ii. Kujumuisha na kuhuisha masuala ya ulinzi wa mtoto kwenye Sera, Sheria na Mitaala ya elimu katika vyuo vya elimu, shule za msingi na sekondari;

iii. Kuratibu utekelezaji wa miongozo na nyaraka za elimu zinazohusu ulinzi na usalama wa mtoto shuleni;

iv. Kufanya tathmini, kutoa taarifa na mrejesho kwa wadau kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule; na

v. Kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuwezesha uratibu na utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni.

## 3.3. Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)

Majukumu yafuatayo yatasimamiwa na Katibu Mkuu OR - TAMISEMI chini ya Idara ya Usimamizi wa Elimu;

i. Kusambaza na kutoa elimu kuhusu Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule kwa kushirikiana na wizara za kisekta;

ii. Kuratibu na kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni kwa kushirikiana na wizara za kisekta;

iii. Kuratibu ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule kwa kushirikiana na wizara za kisekta;

iv. Kuratibu upatikanaji wa taarifa za robo mwaka kutoka tawala za mikoa na kuwasilisha katika wizara yenye dhamana ya watoto na wizara nyingine za kisekta;

v. Kutoa mrejesho kwa wadau kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule; na

vi. Kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuwezesha uratibu na utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule.

## 3.4. Wadau wa Maendeleo

Majukumu yafuatayo yatasimamiwa na Katibu Mkuu mwenye dhamana ya kusimamia maendeleo ya mtoto

i. Kutoa ushauri wa kitaalamu na mchango wa rasilimali kwa ajili ya uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule;

ii. Kuwezesha mafunzo kwa wataalam katika ngazi ya taifa, mkoa, halmashauri, shule na jamii kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari;

iii. Kushiriki katika maandalizi ya vitini na mada za kutolea mafunzo kwa walimu na wanafunzi shuleni.

iv. Kushiriki katika shughuli za utekelezaji, ufuatiliaji na tathimini ya majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule.;

v. Kufanya uchechemuzi na kushiriki katika uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule;

vi. Kushirikiana katika kuhuisha Sera, Sheria, na Mitaala ya uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule;

## 3.5. Tawala za Mikoa

Majukumu yafuatayo yatafanywa na Ofisi ya Afisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii na yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa chini ya Ofisi ya Afisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii.

i. Kusambaza Mwongozo na kutoa elimu kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule ndani ya mkoa na kuoanisha na miongozo mingine ya ulinzi na usalama wa mtoto shuleni;

ii. Kuratibu na kusimamia uanzishaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari zilizopo kwenye maeneo yao;

iii. Kuratibu usimamizi na ufuatiliaji wa kisekta katika utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule;

iv. Kuratibu uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika ngazi ya mkoa kulingana na utaratibu wa MTAKUWWA na kuzipeleka ngazi ya Taifa; na

v. Kuratibu ushiriki wa wadau na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule ngazi ya Mkoa.

## 3.6. Mamlaka za Serikali za Mitaa

### 3.6.1. Halmashauri

Majukumu yafuatayo yatafanywa na Afisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii na yatasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri chini Afisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Ustawi wa Jamii**.**

i. Kusambaza Mwongozo na kutoa elimu ya uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule katika ngazi ya Halmashauri na kuoanisha na miongozo mingine ya ulinzi na usalama wa mtoto shuleni;

ii. Kusimamia uanzishaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari ngazi ya halmashauri;

iii. Kukusanya taarifa za shughuli za Dawati kulingana na utaratibu wa MTAKUWWA na kuziwasilisha mkoani;

iv. Kuratibu mafunzo kwa walimu wa malezi na ushauri nasihi kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto shuleni; na

v. Kuratibu ushiriki wa wadau na upatikanaji wa raslimali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule ngazi ya halmashauri.

### 3.6.2. Kata

Majukumu yafuatayo yatafanywa na Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Ustawi wa Jamii au Afisa Mtendaji Kata kwa kushirikiana na Afisa Elimu Kata

i. Kusambaza Mwongozo na kutoa elimu kuhusu uanzishaji na

uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule ndani ya kata na kuoanisha na miongozo mingine ya ulinzi na usalama wa mtoto shuleni;

ii. Kuratibu mafunzo kwa walimu wa malezi na ushauri nasihi kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto shuleni ngazi ya kata;

iii. Kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika shule za msingi na sekondari kwenye kata husika kwa kuzingatia maelekezo kutoka halmashauri husika; na

iv. Kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Dawati kulingana na utaratibu wa MTAKUWWA na kuziwasilisha halmashauri.

### 3.6.3. Serikali ya Kijiji/Mtaa

i. Majukumu yafuatayo yatafanywa na Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa au Afisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Elimu Kata kutoa elimu na kuhamasisha jamii kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto;

ii. Kushirikiana na Afisa Mtendaji Kata pamoja na Kamati/Bodi ya shule katika uanzishaji na uendeshaji wa Dawati;

iii. Kuandaa na kutoa taarifa ya mashauri ya masuala ya ukatili dhidi ya watoto ngazi ya Kijiji/Mtaa.

### 3.6.4 Kamati/Bodi ya shule

i. Kusimamia uongozi wa shule kuhusu uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule.

ii. Kuelimisha wazazi na jamii juu ya madhara ya ukatili dhidi ya watoto na umuhimu wa kushiriki katika utekelezaji wa

majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto;

iii. Kuhamasisha jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyotendeka kwenye jamii;

iv. Kushauri mkuu wa shule na walimu wa malezi na unasihi juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni.

### 3.6.5. Mkuu wa Shule

i. Kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa dawati la ulinzi na Usalama wa Mtoto Shuleni.

ii. Kuratibu mafunzo ya walimu wa unasihi na nasaha shuleni..

iii. Kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwa kushirikiana na walimu wa malezi, unasihi na nasaha shuleni.

iv. Kuratibu taarifa ya uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto shuleni na kuiwasilisha kwenye ngazi ya kata.

v. Kufanya tathmini ya uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule kwa kushirikiana na walimu wa malezi, unasihi na ushauri nasaha.

### 3.6.6. Walimu wa Malezi na Unasihi

Kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na nje ya Shule kwa kuzingatia yafuatayo:

i. Kutoa mafunzo kwa wanafunzi juu ya madhara ya ukatili dhidi ya watoto na namna ya kutoa taarifa pindi wanapoona dalili au kufanyiwa vitendo vya ukatili ndani na nje ya shule;

ii. Kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto na namna ya kupokea na kushughulikia taarifa za vitendo vya ukatili kutoka kwa wanafunzi;

iii. Kukusanya na kufanyia kazi taarifa zote zinazowasilishwa kwenye Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule kisha kuzifikisha kwa Mkuu wa Shule;

iv. Kuandaa taarifa ya robo mwaka (kila baada ya miezi mitatu) na kuziwasilisha kwa Mkuu wa Shule;

v. Kufanya tathmini ya uendeshaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule kila baada ya miezi sita;

vi. Kutoa huduma ya kwanza ya msaada wa kisaikolojia na unasihi; na

vii. Kutoa rufaa kwa ajili ya kupata huduma stahiki ikiwemo ushauri nasaha kutoka mamlaka mbalimbali kulingana na tatizo.

### 3.6.7. Jamii

i. Kuibua na kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya mtoto vinavyofanyika ndani na nje ya shule;

ii. Kushirikiana na kamati za ulinzi wa wanawake na watoto (MTAKUWWA) zilizopo katika jamii kwenye masuala ya kutokomeza ukatili dhidi ya watoto;

iii. Kutoa msaada wa hali na mali kwa watoto walio katika mazingira hatarishi ili waweze kuendelea na masomo;

iv. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kushughulikia mashauri ya ulinzi na usalama wa mtoto.

### 3.6.8. Viongozi wa Dini /Taasisi za Dini

i. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa malezi bora ya familia na madhara ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

ii. Kushiriki katika kutoa huduma za ushauri na unasihi kwa watoto na familia zao.

iii. Kutoa huduma mbalimbali za msaada, malazi, matibabu na za kisaikolojia.

### 3.6.9. Marafiki wa Elimu

i. Kushirikiana na jamii katika kulinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili ndani na nje ya shule;

ii. Kuibua viashiria na matukio ya ukatili dhidi ya watoto ndani na nje ya shule kupitia Dawati na kutoa taarifa kwa uongozi wa shule husika;

iii. Kushauri wazazi/walezi na watoto katika ngazi ya jamii namna ya kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto;

iv. Kufuatilia rufaa za mashauri kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na

v. Kuhakikisha wazazi/walezi na watoto wanapatiwa huduma za ushauri na unasihi pale ambapo unahitajika.

# Sura ya Nne:

## Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini

## 4.1. Uratibu

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itaratibu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR- TAMISEMI) na wizara nyingine za kisekta kwenye utekelezaji wa Mwongozo huu katika ngazi ya Taifa. Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI itaratibu utekelezaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule katika Mikoa na Halmashauri na mfumo mzima wa ukusanyaji wa taarifa za ukatili dhidi ya watoto kutoka katika shule za msingi na sekondari, serikali za Vijiji/Mitaa kupitia mfumo wa uratibu na ufuatiliaji wa MTAKUWWA.

## 4.2. Ufuatiliaji

Ufuatiliaji wa utendaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule utafanyika kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa na unalenga kupata taarifa za mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itaunda timu ya ufuatiliaji kwa kuhusisha wizara za kisekta na kufanya ufuatiliaji mara mbili kwa mwaka.

Maeneo ya ufuatiliaji yatajumuisha shule za msingi na sekondari, Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji/Mtaa, Ofisi ya Mtendaji wa Kata, Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa.

Aidha, Ufuatiliaji utafanyika kwa Mratibu wa MTAKUWWA ngazi ya Mkoa kubaini iwapo taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule zinawasilishwa kwa wakati na kufanyiwa kazi.

Ufuatiliaji ni jukumu la kila siku kwa kila mdau kwenye eneo lake la utendaji kwa kuzingatia mifumo iliyopo ya ufuatiliaji na utendaji kazi ya wataalam husika. Takwimu na taarifa za ufuatiliaji zitasaidia

katika kufanya tathmini, kupata mrejesho wa utendaji na kufanya maamuzi katika ngazi husika.

Ufuatiliaji utafanyika kila mara katika ngazi zote, ambapo ngazi ya Taifa mara moja (1) kwa mwaka, Mkoa maratatu kwa mwaka (3) Halmashauri, na Kijiji/Mtaa mara tatu (3) kwa mwaka. Timu ya Mkoa itaundwa na Katibu Tawala na itajumuisha wataalam kutoka kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Idara ya Elimu.

Aidha, kwa ngazi ya Halmashauri timu ya ufuatiliaji itaundwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ambayo itahusisha wataalam kutoka katika idara za Mipango, Ufuatiliaji na Takwimu, Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Elimu.

Taarifa za ufuatiliaji za kila robo mwaka zitakuwa sehemu ya taarifa ya utekelezaji wa MTAKUWWA katika ngazi zote na zitafuata utaratibu uliopo wa kutolea taarifa unaoratibiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI na hatimaye kufikishwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

## 4.3. Tathmini

Tathmini ya utendaji wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule itafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) na itaratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kila mwaka kwa kuhusisha wataalamu wa wizara za kisekta, Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

# HITIMISHO

Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule umeandaliwa kwa ajili ya kuimarisha afua za ulinzi na usalama wa mtoto, pia kwa kuzingatia miongozo mingine ikiwemo Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto Shuleni na katika Vyuo vya Ualimu uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mwongozo wa Uendeshaji wa Sanduku la Maoni shuleni uliotolewa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Mwongozo huu ni jukwaa rasmi linalotoa fursa kwa watoto kukutana, kujadili, kutoa taarifa kuhusu masuala ya maendeleo na ustawi wao ikiwemo kutokomeza vitendo vya ukatili na kupata msaada stahiki. Aidha, Mwongozo huu utatumiwa na wadau mbalimbali kutekeleza afua za ulinzi wa watoto shuleni, kwenye jamii na nyumbani ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mipango mikakati ya Taifa ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto.

hakielimu

PLAN INTERNATIONAL

Save the Children